

## MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



### TAARIFA KWA UMMA

7 MACHI, 2018

#### TAARIFA YA KUTOKEA KWA MLIPUKO WA UGONJWA WA “*LISTERIOSIS*” NCHINI AFRIKA KUSINI UNAOTOKANA NA UCHAFUZI WA BAKTERIA KATIKA BIDHAA ZITOKANAZO NA NYAMA

1. Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) imepata taarifa ya kutokea mlipuko wa ugonjwa uitwao *Listeriosis* katika nchi ya Afrika Kusini ambao umehusishwa na ulaji wa bidhaa za nyama zenye uchafuzi wa bakteria aina ya *Listeria monocytogenes*. Taarifa iliyotolewa imeeleza kuwa baadhi ya watu nchini Afrika Kusini wameripotiwa kuugua na wengine kupoteza maisha kutokana na ugonjwa huo.
2. Aina ya bidhaa za nyama zilizohusishwa na mlipuko huo ni pamoja na *sausages* na *polony* aina ya *Viennas*, *Russians*, *Frankfurters* ambazo husindikwa na Makampuni ya *Enterprise Food Production* na *Rainbow Chicken limited* ya nchini Afrika Kusini.
3. Kwa kuwa bidhaa za nyama kutoka Afrika Kusini huingizwa na kuuzwa hapa Tanzania na ili kulinda afya ya walaji, **TFDA imesitisha utoaji wa vibali vya uingizaji nchini wa bidhaa za nyama kutoka nchini Afrika Kusini kuanzia tarehe 7 Machi, 2018 hadi hapo itakapothibitishwa na mamlaka za udhibiti za nchi hiyo kuwa bidhaa hizo ni salama.**
4. TFDA kupitia mifumo yake ya udhibiti wa chakula inaendelea kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa kina ili kubaini uwepo wa bidhaa hizo katika soko na kuzuia uuzwaji wake, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua zaidi kwa mujibu wa sheria.
5. TFDA inatoa wito kwa yeyote atakayebaini uwepo katika soko la Tanzania wa bidhaa tajwa kutoka Afrika Kusini kuacha kuzitumia na kutoa taarifa ofisi za TFDA Makao Makuu na ofisi za Kanda zilizopo Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Dodoma, Mtwara na Tabora au kupitia barua pepe ya [info@tfda.go.tz](mailto:info@tfda.go.tz) au Ofisi za Afya za Halmashauri.
6. Wananchi wanahimizwa kuendelea kushirikiana na TFDA katika kutoa taarifa pindi wanapokuwa na mashaka juu ya usalama na ubora wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa wakati.

Imetolewa na:

**Kaimu, Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Chakula na Dawa**  
**S.L.P 77150**  
**Dar es Salaam**  
[www.tfda.go.tz](http://www.tfda.go.tz)  
[Piga simu bila malipo: 0800110084](tel:0800110084)